MWITO PROG 1100 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 6: 13,14,15.

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1100 kutoka studio zetu za Nairobi.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini mkubwa wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake Harod Williams.Naamini umechukua kalamu na karatasi ili kunakili nasaha utakazozipata kwenye somo la leo.

Kwenye kipindi kilichopita tuliongelea akubwa kuhusu jinsi ya kuishi maisha ya ukristo.Kwa wale ambao hamukuwa nasi kweye somo lililopita tulisoma aya za 13 na 14 za sura ya 6 ya Warumi.

wala msiendelee kuvitoa vungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi,bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki.

Sasa tunaingia kipindi nambari -:1100 na somo letu litazingatia aya ya 14 ambayo tutaisoma…Kwa maana dhambi hautatawala ninyi,kwa sababu hamwi chini ya sheria,bali chini ya neema.

Msikilizaji wangu aya tulizosoma za 11,12 na 13 ….Ni muhimu sana kwa ufahamu wa somo letu.Ni muhimu pia kwa maisha ya ukristo kwa kuwa hapana haja ya dhambi kututawala tena,yule mtu wa zamani,kwa kuwa tumekufa kwa dhambi.Hilo twapaswa kuliweka nyoyoni mwetu na kulikariri kila wakati.Naomba turudi nyuma kidogo kwenye aya ya 11… Vivyo hivyo ninyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Yesu Kristo.

Hilo twapasa kulichukulia vile lilivyo.Hiyo ni kweli kwa kuwa ni hakikisho kutoka kwa mtume Paulo ambaye aliandika maneno hayo chini ya mwongozo wa Roho mtakatifu katika siku ngumu za mateso kwa wakristo.Wakati wa kanisa la kwanza la waaminio.Huo ulikuwa ufunuo wa kuwatia moyo wakristo. Ufunuo huo unadhibitiwa na ukweli kuwa Yesu Kristo mwana wa Mungu alikuja hapa duniani ,akaishi nasi na kuhubifri kuhusu ufalme wa MUngu ,akauawa na kuzikwa na kufufuka siku ya tatu. .Alilipa kikamilifu deni la dhambi zilizokumba binadamu.Inabidi tulibinafsishe neno la Mungu ,hasa kufa kwa dhambi na kulitekeleza maishani mwetu ,kwa nguvu za Roho mtakatifu ,ndipo kufa kwetu kwa dhambi kudhihirike kwa ulimwengu.Ikiwa umekufa kwa dhambi hutaruhusu dhambi iwe Bwana katika maisha yako ,kwa kuwa itakutumikisha kama vile bwana afanyavyo kwa mtumwa wake au jinsi mfalme atawalavyo taifa.Maandiko yamesema tusiruhusu miili yetu kutumika kama viungo kwa dhambi.Kumbuka mfano ulio kwenye injili ya Mathayo,ambapo mtu mmoja alitubu dhambi zake na kuisafisha nyuma yake na kuanza kuishi maisha yampndezayo Mungu ,lakini baada ya muda akaruhusu dhambi kuingia,ambapo mapepo waliitana ,wakiwemo wale wabaya zaidi kuja kufanya kambi ndani ya huyu mtu.Ikiwa hutajitoa kwa dhambi ,basi utajitoa kwa Mungu ,lakini usipojitoa kwa Mungu ,basi inamaanisha umejitoa kwa shetani na viungo vyako vitatumika kwa ajili ya ibilisi. Ukifa kwa dhambi ,unakuwa hai kwa Mungu.Na hivyo ndivyo ilivyo hapana namna nyingine.Aya ya 14 inasema: Kwa maana dhambi haitatawala ninyi,kwa sababu hamwi chini ya sheria,bali chini ya neema.

Ukiruhusu dhambi maishani mwako itakutawala,lakini kumbuka kuwa huko chini ha sheria ,bali chini ya neema ,ambayo kwao tulipata wokovu.Kumbuka mtu tuliyezungumzia aiyeruhusu ibilisi kuitaka na

kupiga kambi ndani yake ,alikuwa ameacha nyumba yake safi ,lakini hakujaza ndno la Mungu.Aliendekeza dhambi na mapepo wakafahamu hivyo na kuitaka na kupiga kambi ndani yake.Nuvu za roho mtakatifu zapasa upatiwa nafasi yake ndani yako ili kukuwezesha kuishi maisha ya ushindi.Mungu mwenyewe ndiye aliyetoa ahadi hiyo kwamba dhambi isikutawale,kwa kuwa huko chini ya sheria bali neema ambayo kwayo tulipata wokovu kwa njia ya imani.Neno tupu lisilo na uhai huuwa ,bali roho ndiye atupaye uzima.Kifo cha Yesu msalabani kilivunja ngome na kukata minyororo ya dhambi iliokuwa imetufunga.Damu ya Yesu ilitukomboa na kutuweka huru.Neema ya Mungu ni kuu nay a ajabu.Naomba nikomee hapa kwa leo ,lakini natoa mwito kwako ikiwa hujampokea Kristo kuwa mswokozi wako ,wakati ni huu.

Ninasubiri uchukue hatua hiyo ya kumwalika Kristo kuwa mwokozi wako,kisha uniandikie au unitumie ujumbe mfupi.Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1100 Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 14 &15 za sura ya 6 ya kitabu cha Warumi.Hni mimi ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mibaraka na neema tele zake Mungu.Kwaheri.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxoooooxxxxxxxxxxxxxxxvvvv